



TAARIFA KWA UMMA

MAKUSANYO YA KODI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI - SEPTEMBER 2026) KATIKA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Zanzibar, 02 Oktoba, 2026:

1. MAKUSANYO YA SEPTEMBER 2026

Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), unayo heshima ya kuwataarifu Walipakodi pamoja na Wananchi wote wa Zanzibar kwamba katika Mwezi wa Septemba 2026, ZRA ilikadiriwa kukusanya Jumla ya **Tshs.128.006 Bilioni**, na **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 128.098 Bilioni**, ikijumuisha Mapato ya kodi na Mapato yasio ya Kodi, makusanyo hayo ni **UFANISI** wa **asilimia 100.10** wa Makadirio.

Aidha, Makusanyo halisi ya Mwezi Septemba kwa Mwaka wa Fedha uliopita wa 2025/2026, yalikuwa ni **Tshs 109.498 Bilioni**, ambayo yakilinganishwa na Makusanyo halisi ya Septemba ya Mwaka huu wa Fedha wa 2026/2027, yanaonesha **UKUAJI** wa Makusanyo halisi wa **asilimia 16.99** (Jedwali Na. 1 linatoa ufafanuzi zaidi).

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Mwezi wa Septemba kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027.

	2025/2026	2026/2027				
Mwezi	Makusanyo (Tshs. Bilioni)	Makisio (Tshs. Bilioni)	Makusanyo (Tshs. Bilioni)	Ufanisi (%)	Ongezeko (Tshs. Bilioni)	Ukuaji (%)
Septemba	109.498	128.006	128.098	100.10	18.599	16.99

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar, 2026.

2. MAKUSANYO YA KODI KWA ROBO YA KWANZA (JULAI - SEPTEMBER 2026)

Aidha, ZRA inapenda kutoa taarifa kwamba katika kipindi cha Robo ya Kwanza (Julai – Septemba 2026) ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, ZRA ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 351.106 bilioni** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2026 imefanikiwa kukusanya Jumla ya **Tshs. 353.310 Bilioni** ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 100.63** ya Makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa.

Makusanyo haya, yanapolinganishwa na Makusanyo halisi ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Julai – Septemba 2025) ambayo yalikuwa ni **Tshs. 274.291 Bilioni** yanaonesha kuwa kuna ongezeko la Makusanyo ya **Tshs. 79.019 Bilioni**, sawa na **UKUAJI** wa **asilimia 28.81** (Jedwali Na. 2 linatoa ufafanuzi zaidi).

Jedwali Na. 2: Makusanyo ya Mapato kwa mlinganisho wa vipindi viwili Robo ya kwanza (Julai - Septemba) kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027.

	2025/2026	2026/2027				
Mwezi	Makusanyo (Tshs. Bilioni)	Makisio (Tshs. Bilioni)	Makusanyo (Tshs. Bilioni)	Ufanisi (%)	Ongezeko (Tshs. Bilioni)	Ukuaji (%)
Julai	73.942	107.779	108.082	100.28	34.139	46.17
Agosti	90.851	115.321	117.131	101.57	26.279	28.93
Septemba	109.498	128.006	128.098	100.07	18.599	16.99
Jumla	274.291	351.107	353.310	100.63	79.019	28.81

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar 2026

3. SABABU ZA MAFANIKIO KATIKA UKUSANYAJI:

Ukuaji wa Makusanyo ya Kodi kwa **asilimia 28.81** kwa kipindi cha Julai – Septemba 2026, pamoja na mambo mengine umesababishwa na:-

- Kuimarika** na Kustawi kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na Sera na uongozi mzuri wa **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, zilizoimarisha mazingira ya biashara kwa pande zote mbili za Muungano na kupelekea kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma kutoka na kwenda pande zote za Muungano.
- Uwekezaji** mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na upanuzi wa huduma za kijamii ambazo zimesaidia kufungua fursa nyingi za kiuchumi ndani ya Zanzibar kufuatia utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**,
- Kuimarisha** programu mbalimbali za elimu kwa walipakodi, hususani zinazolenga kutoa uelewa kuhusu mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu za kodi, ili kuhakikisha walipakodi wanafahamu kwa wakati wajibu wao, haki zao na matakwa mapya ya kisheria.
- Kuendelea** kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato ikiwemo matumizi ya **mfumo wa Risiti za Kielektroniki (VFMS)**, na matumizi ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa ZIDRAS, ambapo Mfumo wa VFMS sasa unaweza kutoa risiti kwa kuonesha Mahala biashara ilipo (Location) na Mfumo wa ZIDRAS kuweza kutoa taarifa sahihi za wafanya biashara wasiotumia mfumo kikamilifu. Aidha ZRA imeongeza takwa la kisheria la kuwataka watoa huduma wote wa malazi ZANZIBAR kutumia Mifumo ya uendeshaji wa shughuli za malazi (Property Management System) na kuunganisha Mifumo hiyo na Mifumo ya ZRA.
- Usimamizi** wa Weledi, Maadili na Uwajibikaji kwa wafanyakazi wa Mamlaka kupitia utoaji wa mafunzo endelevu ndani na nje ya nchi yanayolenga kuongeza ujuzi, kuimarisha nidhamu ya kazi na kujenga utamaduni wa uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu

4. MIKAKATI YA UKUSANYAJI KWA ROBO YA PILI (Oktoba – Disemba 2026):

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi kwa Robo ya Pili ya Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 (Oktoba - Disemba 2026), ZRA itaendelea kutekeleza yafuatayo:-

- Kuimarisha** na Kuendeleza Programu za Elimu kwa Walipakodi na makundi mbalimbali ili kuongeza uelewa kuhusu sheria, kanuni, taratibu za kodi, pamoja na haki na wajibu wao, na hivyo kuhamasisha uzingatiaji wa sheria na ulipaji wa kodi kwa hiari. Programu hizo zinatekelezwa kupitia ziara za kitaaluma, vipindi vya radio na televisheni, semina, mikutano na majadiliano na makundi mbalimbali ya Walipakodi.
- Kuendeleza** mazoezi maalum ya ufuatiliaji wa Walipakodi kwa kuhimiza matumizi sahihi ya Mfumo wa Risiti za Kielektroniki (VFMS), kuunganisha mifumo ya TEHAMA ya ZRA na biashara, na kuhakikisha biashara zote zinazofanya shughuli Zanzibar, zikiwemo za kidijitali, zinasajiliwa na kulipa kodi stahiki.

- iii. **Kuendelea** na **Kuimarisha** Mkakati wa Klabu za Kodi kwa kuongeza idadi ya skuli zenye Klabu za Kodi na kuendelea kutoa elimu ya kodi ili kujenga kizazi chenye uelewa wa umuhimu wa kodi.
- iv. **Kuendelea kusogeza huduma** za kodi karibu na wananchi kwa kuendesha Kambi Maalum za Kodi (Tax Clinics) katika maeneo mbalimbali, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari.
- v. **Kuendeleza Mashirikiano** na Jumuiya , Taasisi na makundi mbali mbali ya Wafanyabiashara katika kushajihisha ulipaji Kodi wa Hiyari.

5. HITIMISHO:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inaendelea kutoa shukurani kwa walipakodi wote kwa uwajibikaji na moyo wa kulipa kodi kwa hiari katika Robo ya kwanza Mwaka wa fedha 2026/2027. ZRA inawahimiza walipakodi kuendeleza ari hiyo ili kufanikisha na kuvuka lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na hivyo kuiwezesha Serikali kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Aidha, Mamlaka inaishukuru Serikali kwa usimamizi na miongozo inayotolewa, pamoja na Taasisi za Umma na wadau mbalimbali kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya ukusanyaji wa mapato.

ZRA itaendelea kusimamia Sheria za Kodi ili kurahisisha biashara za Walipakodi pamoja na kuimarisha mahusiano mema yatakayopelekea ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na sambamba na kuiwezesha Serikali kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii.

“Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar”



MAKAME KHAMIS MOH'D

**MKUU WA KITENGO CHA HABARI, UHUSIANO NA HUDUMA KWA WATEJA
MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR**